



# NISHATI

HABARI ZA  
NISHATI

## News *Bulletin*

[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz) [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara ya Nishati) [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania) [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017) [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara ya Nishati)

Toleo Namba 37

Aprili 1 - 30, 2022

## WAZIRI MAKAMBA AELEZA MAFANIKIO YA SEKTA YA NISHATI NA MIKAKATI YA KUENDELEZA SEKTA



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA  
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au  
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma

# BODI YA UHARIRI

## Mwenyekiti

**Mhandisi Felchesmi Mramba**  
Katibu Mkuu

## Makamu Mwenyekiti

**Kheri Mahimbali**

## Mhariri

**Dorina G. Makaya**

## Waandishi

Teresia Mhagama  
Zuena Msuya  
Hafsa Omar  
Timotheo Mathayo

## Msanifu Kurasa

Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu  
namba +255-26-2322018  
Nukushi: +255-26-2320148  
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano  
Mitumba Dodoma,  
S.L.P 2494, Dodoma



 [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

 [Wizara ya Nishati](#)

 [@Nishati2017](#)

 [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](#)

 [Wizara ya Nishati](#)

# WAZIRI MAKAMBA AELEZA MAFANIKIO YA SEKTA YA NISHATI NA MIKAKATI YA KUENDELEZA SEKTA



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akizungumza katika Kipindi cha Mwaka Mmoja wa Mama kinachorushwa na Azam TV kuhusu mafanikio ya Sekta ya Nishati Katika Mwaka Mmoja wa Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Machi 24, 2022 mkoani Dar es Salaam.

## **Teresia Mhagama na** **Zuena Msuya**

**W**aziri wa Nishati, Mhe. January Makamba ametaja mafanikio mbalimbali ya Sekta ya Nishati yaliyofikiwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha mwaka mmoja.

Mafanikio hayo aliyataja tarehe 24 Machi, 2022 wakati akizungumza na Wahariri wa Vyombo mbalimbali vya Habari na wanazuoni jijini Dar es Salaam.

Mafanikio aliyoyataja ni

pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuhamishiwa Wizara ya Nishati ambapo imeimarishwa na kufanyiwa mabadiliko kadhaa ya kikanuni na kiuendeshaji yanayoweza Taasisi hiyo kudhibiti kwa weledi sekta nyeti ya umeme na mafuta.

Wakala wa Nishati Vijijini (REA) umewekwa kwenye nafasi yake, kwani haujikiti katika umeme pekee bali na nishati nyingine ikiwemo ya kupikia, mafuta na nyinginezo na kwa sasa imebuniwa miradi mingine ya nishati na hasa nishati ya kupikia ambayo ndiyo nishati namba moja hapa nchini.

Alieleza kuwa, katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita imeundwa

programu kubwa ya kuhakikisha kwamba inapatikana nishati safi ya kupikia, salama na ya bei nafuu ambapo programu hiyo itazinduliwa wakati wa Bajeti ya Wizara ya Nishati ya mwaka 2022/2023.

Kuhusu upatikanaji wa mafuta vijijini, alisema yanafanyika mabadiliko ya kanuni ili kurahisisha ujenzi wa vituo vidogo vya mafuta vijijini ili hata kama mwananchi anataka lita moja ya mafuta awapo kijijini, awekewe mafuta yaliyo safi na ya bei nafuu.

Aidha alieleza kuwa, Wizara ya Nishati imeandaa programu kubwa ya kupeleka umeme vitongojini na kazi kubwa inayofanyika sasa ni usimamizi makini wa miradi hii ya umeme vijijini inayoendelea ili ifanyike kwa ufanisi.

Katika mikakati ya kuleta unafuu wa bei ya gesi ya mitungi nchini, Waziri Makamba alieleza kuwa, ndani ya mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali imepata wawekezaji na eneo ili kuweza kushusha meli ya angalau tani Elfu 45 ambayo itasaidia gesi iingie kwa wingi na iwe nabei nafuu.

Aliongeza kuwa, Mwezi wa Nne mwaka huu atakaa na wauzaji wa gesi ili kuona namna ambavyo mfumo wa biashara unaweza kubadilishwa ili kurahisisha ufikaji wa gesi katika maeneo mengi nchini hivyo

## WAZIRI MAKAMBA AELEZA MAFANIKIO YA SEKTA YA NISHATI NA MIKAKATI YA KUENDELEZA SEKTA

kuleta unafuu wa bidhaa hiyo.

Kuhusu usambazaji gesi, alisema kuwa, Katika mwaka ujao wa fedha imewekwa bajeti ya kujenga vituo mama na vituo dada kwa ajili ya kujaza gesi ya kwenye magari na kushirikiana na pia kushirikiana na REA na TPDC katika mradi wa kusambaza gesi majumbani katika njia ya bomba la gesi kutoka Dar es Salaam hadi Mtwara.

Vilevile, kuhusu uhifadhi wa mafuta, alisema kuwa kuna changamoto ya miundombinu ya kuhifadhi na kushusha mafuta ambayo imeanza kufanyiwa kazi na Serikali imeanza

mazungumzo na makampuni makubwa kuhakikisha kuwa inawekwa miundombinu bora ya kupakia mafuta, kuyahifadhi na kupakua tena ili kuyasafirsha nchi jirani.

Alizungumzia pia hifadhi ya mafuta ya kimkakati ambapo alieleza kuwa, zinaandaliwa kanuni mpya kwa ajili ya kuwa na hifadhi hiyo na kwamba Serikali inatambua kuwa sekta binafsi ina umuhimu katika kuhakikisha kuwa suala hilo linafanikiwa.

Kuhusu shughuli za udhibiti wa mkondo wa juu wa Petroli, Waziri wa Nishati alieleza kuwa, uongozi na utendaji wa

Taasisi inayosimamia mkondo huo (PURA) imeimarishwa na katika kipindi cha mwaka mmoja yamefanyika maandalizi makubwa ya kwenda kwenye tenda mwakani kwa ajili ya uwekezaji kwenye utafiti na kutafuta mafuta katika vitalu vilivyopo nchini ambapo mara ya mwisho Tanzania ilishiriki tenda hiyo mwaka 2013.

Alitanabaisha kwamba, PURA pia imeendelea kusimamia masuala mbalimbali katika Sekta ya Mafuta na Gesi kwa kwa umakini ikiwemo mikataba mbalimbali katika sekta ya gesi ili kuhakikisha kuwa gharama zinazosemwa na wawekezaji kuwa zimetumika katika uwekezaji huo nchini ni gharama halisi.

Kuhusu upatikanaji na usambazaji wa umeme nchini, alisema kuwa, mradi wa umeme wa Julius Nyerere wa megawati 2115, unaendelea kutekelezwa kwa mafanikio makubwa na kwa sasa mfumo wa usimamizi umebadilishwa kwani unasimamiwa kisayansi na Mhe. Rais, Samia Suluhu Hassan ameidhinisha fedha nyingi za kutekeleza mradi huo.

Alisema mradi huo una maeneo manne yanayoenda sambamba ambayo ni ujenzi wa bwawa, ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka eneo la mradi hadi Chalinze mkoani Pwani, ujenzi wa kituo



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (kushoto) akionyesha takwimu za matumizi ya umeme nchini katika Kipindi cha Mwaka Mmoja wa Mama kinachorushwa na Azam TV kuhusu mafanikio ya Sekta ya Nishati Katika Mwaka Mmoja wa Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Machi 24, 2022 mkoani Dar es Salaam.

## WAZIRI MAKAMBA AELEZA MAFANIKIO YA SEKTA YA NISHATI NA MIKAKATI YA KUENDELEZA SEKTA



*Baadhi ya Wahariri wa Vyombo vya Habari na wanazuoni wakiwa katika Kipindi cha Mwaka Mmoja wa Mama kinachorushwa na Azam TV ambapo Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba alikuwa akizungumza kuhusu mafanikio ya Sekta ya Nishati Katika Mwaka Mmoja wa Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Machi 24, 2022 mkoani Dar es Salaam.*

cha umeme Chalinze na mradi wa matoleo kutoka chalinze-DSM- Tanga na Dodoma.

Alieleza kuwa, katika mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali imesaini mikataba ya kutekeleza miradi ya usafirishaji umeme kutoka eneo la mradi wa Julius Nyerere hadi Chalinze na kutoa umeme kutoka Chalinze kwenda maeneo mengine na sasa Serikali iko mbioni kusaini mkataba wa matoleo ya umeme

kutoka kituo cha Chalinze.

Kuhusu upatikanaji wa umeme alisema kuwa, umeme unaopatikana ni megawati 1700 ambazo ni ndogo hivyo Serikali imeanzisha, kubuni na kuendeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji umeme itakayofikisha megawati 5000 ifikapo mwaka 2025.

Kuhusu Jotoardhi alisema kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita imeamua kushirikiana na washirika wa maendeleo ili

kupata maeneo ya uhakika ya upatikanaji wa Jotoardhi na yakithibika kwamba yanaweza kuzalisha umeme nchi itaingia katika uzalishaji.

Aidha, kuhusu Nishati Jadidifu, alisema kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha utayarishaji na uanzaji wa utekelezaji wa takribani megawati 900 za umeme utakaotokana na upepo na jua ambazo zitaingizwa kwenye gridi ya Taifa.

# Mradi wa JNHPP wafikia asilimia 56

■ Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yapongeza



Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba akizungumza na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakati walipotembelea Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere tarehe 16.03.2022 mkoani Pwani.

**W**aziri wa Nishati, January

Makamba ameeleza kuwa, utekelezaji wa Mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) utakaozalisha umeme wa kiasi cha megawati 2115, kwa sasa umefikia asilimia 56 na kwamba Serikali inaendelea kuhakikisha kuwa mradi huo unatekelezwa kwa

kasi, uadilifu, ubora na viwango vinavyotakiwa ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Waziri Makamba aliyasema hayo tarehe 16 Machi, 2022, Rufiji mkoani Pwani wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyolenga kukagua utekelezaji wa mradi huo.

Alieleza kuwa, mradi huo kwa sasa unatekelezwa kwa kasi

kutokana na maboresho mbalimbali yaliyofanyika katika usimamizi na uendeshaji wa mradi huo ambapo alitaja baadhi ya maboresho hayo kuwa ni kuongeza utaalam na wataalam pia Mkandarasi wa mradi huo, ambaye ni kampuni ya Elsewedy Electric amehimizwa kuongeza wataalam wenye uzoefu wa usimamizi wa miradi mikubwa kama wa JNHPP.

Alitaja maboresho mengine kuwa ni mabadiliko ya uongozi katika mradi, kubadili mfumo wa mawasiliano kati ya Wizara na TANESCO pamoja na TANESCO na Mkandarasi pamoja na mabadiliko ya Menejimenti na Bodi ya TANESCO ambayo yamekuja na mbinu za kisayansi za kutekeleza mradi huo na matunda yake yameanza kuonekana.

# Mradi wa JNHPP wafikia asilimia 56



Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba akizungumza na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakati walipotembelea mradi wa Ujenzi wa Bwawa la kufua umeme wa maji la Julius Nyerere tarehe 16.03.2022 mkoani Pwani

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakipata maelezo kuhusu maendeleo mbalimbali ya mradi wa ujenzi wa Bwawa la kufua umeme walipotembelea tarehe 16.03.2022 Mkoani Pwani Wilayani Rufiji mkoani Pwani

Aliongeza kuwa, kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita mradi ulikuwa chini ya asilimia 40 lakini sasa umefikia asilimia 56 na kwamba na kwa upande wa malipo kwa Mkandarasi, mwaka jana malipo yaliyofanyika yalikuwa ni takriban shilingi Trilioni Mbili na hadi sasa malipo yaliyokwishafanyika ni shilingi Trilioni 3.4.

Kutokana na hayo, alitoa shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ambaye amedhamiria katika kuhakikisha kuwa mradi huo unatekelezwa ili nchi iweze kuwa na umeme wa uhakika ambapo amekuwa akiidhinisha fedha zinazotolewa na Serikali ili kutekeleza

mradi huo.

Waziri Makamba alieleza kuwa, ujenzi wa Bwawa la umeme katika mradi wa JNHPP unaenda sambamba na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka kwenye bwawa kwenda Chalinze mkoani Pwani (km 160), kujenga kituo cha kupoza umeme Chalinze na kujenga mradi wa upanuzi wa gridi ya Taifa kwa upande wa Kaskazini Mashariki mwa Tanzania ambapo mradi huo utatoa umeme kutoka Chalinze na kupeleka Kinyerezi, Mkuranga, Kigoma, Segera na Tanga na hivyo kuwezesha umeme huo kusambazwa katika maeneo mabalimbali nchini.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati

ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula alieleza kuwa, Kamati hiyo imekagua mradi huo ikiwa ni ziara ya kikanuni kwani Kamati hiyo inawajibu wa kusimama Wizara kwenye utekelezaji wa shughuli za Kiserikali ambapo moja ya shughuli hizo ni mradi wa JNHPP.

Alisema kuwa, Kamati hiyo imeona kazi kubwa inayofanyika katika mradi huo na kwamba kuna changamoto mbalimbali zimejitokeza lakini wameona kuwa changamoto hizo si za kukatisha tamaa hivyo wana imani kuwa mradi utakamilika kwa wakati.

“Tunaipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa inayofanyika katika

utekelezaji wa mradi huu kwani unafanyika kwa viwango vinavyotakiwa na mkandarasi anaendelea kulipwa fedha kwa wakati hivyo tunaendelea kuiaa Serikali isimamie kwa karibu mradi huu ili matamano ya watanzania ya kuona mradi huu unazalisha umeme yanafikiwa.”

Alisema Kitandula Kamati hiyo ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilitembelea maeneo mbalimbali katika mradi huo ikiwemo eneo la Bwawa Kuu la Kutunza Maji, Daraja la Kudumu, eneo kutakapofungwa mitambo ya kuzalisha umeme na kituo cha kuchochea na kupoza umeme.

# Mradi wa JNHPP wafikia asilimia 56



*Picha mbalimbali za ujenzi wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere utakaozalisha umeme wa kiasi cha megawati 2115.*



# KAGERA KUNUFAIKA NA MRADI WA UJENZI BOMBA LA MAFUTA



Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato akizungumza na wadau waliohudhuria kongamano la kujadili fursa zilizopo kwenye mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Uganda hadi Tanzania (hawamo pichani). Tukio hilo lilifanyika katika Mkoa wa Kagera, ukumbi wa Mkuu wa Mkoa wa Kagera tarehe 07 Machi 2022.

## **Na Timotheo Mathayo, Kagera.**

**S**erikali imewataka wananchi wa Mkoa wa Kagera na Mikoa jirani kuchangamkia fursa zilizopo kwenye mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta (EACOP) kutoka nchi ya Uganda hadi Tanga nchini Tanzania.

Kauli hiyo imetolewa na mkuu wa wilaya ya Bukoba, Moses Machali wakati wa ufunguzi wa kikao cha kujadili maendeleo ya mradi wa ujenzi wa Bomba la

Mafuta kilichofanyika mjini Bukoba katika mkoa wa Kagera Jumatatu Machi 7, 2022.

Amesema lengo la kongamano hilo ni kuwatambulisha wakandarasi, wajenzi wa Mradi huo na kujadili fursa zilizopo kwenye Mradi huu ambao wananchi hawana budi kuzitumia kikamilifu.

Amewataja Wakandarasi hao kuwa ni EALS ambaye atahusika na shughuli ya kusafirisha mabomba, SCHNEIDER ambaye atahusika na masuala ya umeme na CCP

aliyepewa kazi ya ujenzi na Usalama wa bomba.

Machali ametaja wilaya ambazo bomba hilo la mafuta litapita kuwa ni Bukoba, Biharamulo, Misenyi na Muleba ambapo amewataka wafanya biashara na wadau wengine kutumia fursa hiyo ya mradi wa EACOP.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la uwezeshaji wananchi kiuchumi, Benji Issa amesema vifaa vya ujenzi kama mchanga, nondo, kokoto na saruji vitatoka Tanzania katika kipindi chote cha utekelezaji wa

mradi huo.

Fursa zilizopo kwa wananchi na wajasiliamali ni pamoja na biashara ya kuuza chakula, kufanya kazi za muda mfupi kama vibarua wakati wa utekelezaji wa mradi.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato amesema kuwa bomba hilo la Mafuta katika eneo la Tanzania litapita katika mikoa minane ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga.

Ameagiza wataalam kutoka Shirika la mafuta nchini (TPDC) waainishe fursa zilizopo katika mradi wa ujenzi wa bomba hilo la Mafuta kwa kila mkoa ili wananchi wajulishwe mapema.

Serikali ya Tanzania kupitia shirika la TPDC itanufaika kwa kupata asilimia 15 kutoka kwenye mradi huo wa bomba la Mafuta.

Kongamano hilo limehudhuriwa na wataalam kutoka Wizara ya Nishati, TPDC, EWURA, EACOP, Katibu Tawala Mkoa wa Kagera (RAS), Wakurugenzi kutoka Halmashauri ambazo bomba hilo litapita pamoja na wafanyabiashara kutoka mkoa wa Kagera.

## KAGERA KUNUFAIKA NA MRADI WA UJENZI BOMBA LA MAFUTA



Mhe. Moses Machali, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, akifungua Mkutano wa wadau wa Bomba la Mafuta (EACOP) uliofanyika katika Mkoa wa Kagera, tarehe 07, Machi 2022, katika Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa KAGERA ili kuwawezesha wadau kujadili fursa zilizopo kwenye mradi wa bomba la Mafuta pamoja na kuwatambulisha wakandarasi watekelezaji wa mradi huo ambao ni EALS, SCHNEIDER na CCP.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la uwezeshaji wananchi kiuchumi, Benji Issa akizungumza na wadau mbalimbali waliohudhuria Mkutano wa Bomba la Mafuta la EACOP, uliofanyika katika ukumbi wa Mkuu wa Mkoa wa Kagera tarehe 07 Machi 2022.



Wadau mbalimbali waliohudhuria kongamano la kujadili fursa zilizopo kwenye mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Uganda hadi Tanzania, Mkutano huo ulihudhuriwa na wataalam kutoka Wizara ya Nishati, TPDC, EWURA, EACOP, katibu Tawala Mkoa wa Kagera (RAS), wakurugenzi kutoka Halmashauri za Mkoa wa Kagera pamoja na Wafanyabiashara kutoka Mkoa wa Kagera. Tukio tarehe 07 Machi 2022.

## Naibu Katibu Mkuu Nishati, akagua eneo la upakuaji mafuta katika kina kirefu cha Bahari

**N**aibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali amefanya ziara ya kushtukiza ya kukagua eneo la kupakua Mafuta kutoka kwenye Meli

kuingia bandarini katika kina kirefu cha Bahari eneo la Kigamboni jijini Dar es salaam.

Mahimbali amefanya ziara hiyo, Machi 29, 2022 kwa lengo la kujionea shughuli zinavyofanyika katika eneo hilo pamoja

na mazingira ya kufanyia kazi.

Akiwa katika ziara hiyo alikutana na baadhi ya wafanyakazi katika eneo hilo na kuwaeleza kuwa serikali ya inaendelea kuimarisha na kuboresha sekta ya mafuta nchini

ili iweze kuleta tija zaidi kwa taifa na wananchi wake.

Aidha aliwasisitiza wafanyakazi hao kufanya kazi kwa weledi wakizingatia maslahi mapana na nchini yetu.



*Picha mbalimbali zikionyesha ziara ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati (mwenye miwani) katika eneo la upakuaji mafuta katika kina kirefu cha bandari Kigamboni mkoani Dar es Salaam.*

## KAGERA KUUNGANISHWA NA UMEME WA GRIDI



Mhe. Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishati, akikagua alama maalum zitakapojengwa nguzo za kupokea umeme wa Gridi, katika kituo cha kupokelea umeme cha kyaka, kilichopo wilaya ya Misenyi Mkoa wa Kagera, wakati wa ziara ya kukagua maandalizi ya Ujenzi wa Njia ya kusafirisha Umeme kutoka Benako kwenda Kyaka tarehe 4 Machi 2022.

Mhe. Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishati (wanne kutoka kulia) akiwa na wataalam kutoka Tanesco Mkoa wa Kagera, wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama wilaya ya Misenyi, wakati wa ziara ya kukagua maandalizi ya Ujenzi wa Njia ya kusafirisha Umeme kutoka Benako kwenda Kyaka tarehe 4 Machi 2022.

### **Na Timotheo Mathayo, Kagera.**

**S**erikali imeanza maandalizi ya kuunganisha Mkoa wa Kagera kwenye umeme wa Gridi ya Taifa, lengo likiwa ni kufanya Mkoa wa Kagera kupata umeme kutoka Tanzania.

Kauli hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato wakati wa ziara ya kukagua maandalizi ya ujenzi wa njia ya kupitisha umeme kutoka Kyaka kwenda Benako pamoja na kituo cha kupooza umeme cha Kyaka chenye uwezo wa kuzalisha kilovoti 132.

Katika ziara hiyo iliyofanyika Machi 5 mwaka huu amesema kituo cha Kyaka kinapokea umeme kutoka Masaka nchini Uganda na umeme huo ndio unaotumika katika Mkoa wa



**kituo cha Kyaka kinapokea umeme kutoka Masaka nchini Uganda na umeme huo ndio unaotumika katika Mkoa wa Kagera kwa kipindi chote."**

Kagera kwa kipindi chote.

Ametaja kwamba wilaya ya Biharamulo na Ngara zilizopo mkoani Kagera zinatumia umeme wa gridi kutoka Tanzania ambapo wilaya nyingine zilizobaki

zinatumia umeme kutoka Uganda.

Akizungumza na waandishi wa habari Mkoani Kagera, Naibu waziri huyo amesema umeme wa gridi ya Taifa utaanzia Benako, Kyaka.

Aidha ujenzi wa kituo cha umeme cha Nyakanazi umefikia asilimia 90 kabla ya kukamilika ili wananchi waanze kupata huduma ya umeme wa uhakika.

Umeme huo utakaopokelewa kituo cha Nyakanazi utatokea katika vyanzo mbalimbali kama vile Ulyankulu, Geita, Shinyanga, Singida, Dodoma, Iringa na maeneo mengine hapa nchini.

Umeme huo utaanza kupokelewa mjini Geita na kisha kupelekwa Nyakanazi, Kyaka na hatimaye kufikishwa Kibeta kwa ajili ya kusambazwa kila eneo la Mkoa wa Kagera.

Byabato amewataka wakazi

## KAGERA KUUNGANISHWA NA UMEME WA GRIDI



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato, (wakwanza kutoka kulia) akizama ukubwa wa eneo la kituo cha kupokelea umeme cha kyaka kilichopo Mkoani Kagera, wakati wa ziara ya kukagua maandalizi ya Ujenzi wa Njia ya kusafirisha Umeme kutoka Benako kwenda Kyaka.

wa mkoa wa Kagera kujiandaa ili waweze kutoa ushirikiano kwa serikali kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa miundombinu ya kupokelea umeme wa gridi.

Aidha ametaja baadhi ya changamoto za kutumia umeme kutoka nchi jirani ikiwa ni pamoja na kutopata umeme wa kutosha, kushidwa kufanya marekebisho ya njia ya kusambaza umeme na kusafisha kwa wakati.

Hata hivyo amesema umeme wa gridi ya Taifa mkoani Kagera

utaongeza uhakika wa umeme na hivyo kutumika kwa matumizi ya viwanda kama kiwanda cha sukari Kagera.

Meneja usimamizi wa fidia na mazingira kutoka Tanesco, Dkt. Richard Muyungi amesema kuwa njia ya kusafirisha umeme kutoka Benako kuja kyaka ina urefu wa kilomita 170.

Njia hiyo tayari imewekwa alama na uthamini wa mali utaanza kufanyika hivi karibuni na fidia italipwa kuanzia mwezi wa tano mwaka huu.



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato, (wa pili kutoka upande wa kulia) akikagua ukubwa wa eneo, zitakapojengwa nguzo za kupokelea umeme wa Gridi, katika kituo cha kupokelea umeme cha Kyaka, kilichopo wilaya ya Misenyi, Mkoa wa Kagera wakati wa ziara ya kukagua maandalizi ya Ujenzi wa Njia ya kusafirisha Umeme kutoka Benako kwenda Kyaka tarehe 4 Machi 2022.

# Waziri Makamba na Benki ya Dunia wajaadili maendeleo Sekta ya Nishati

## Na Zuena Msuya

**W**aziri wa Nishati January

Makamba amekutana na ujumbe wa Benki ya Dunia (WB) ukiongozwa na Mkurugenzi Mkazi wa benki hiyo kwa upande wa Tanzania, Mara Warwick, na kuzungumzia mambo mbalimbali kubwa likiwa ni uendelezaji wa Sekta Nishati ikiwemo masuala ya umeme na gesi.

Katika mazungumzo hayo, Makamba aliishukuru benki hiyo kwa ushirikiano wake na

Serikali ya Tanzania pia kuwezesha utekelezaji wa miradi ya Maendeleo nchini ukiwemo ule wa Umeme wa kuunganisha Tanzania na Zambia (TAZA).

Mazungumzo hayo yalifanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo mkoani Dar es Salaam, Machi 28, 2022. Pamoja na mambo mengine mazungumzo hayo yamelenga zaidi kuimarisha ushirikiano kati ya benki hiyo na Serikali ya Tanzania katika kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

“Serikali ya Tanzania inaishukuru Benki ya



Waziri wa Nishati January Makamba, akizungumza na Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia kwa upande wa Tanzania, Mara Warwick, (hawapo pichani) wakati wa kikao cha kujadili maendeleo ya miradi ya Sekta ya Nishati, kilichofanyika mkoani Dar Es Salaam, Machi 28, 2022.

Dunia kwa kuwezesha

miradi ya nishati hapa nchini, tunawaahidi tutaendelea kushirikiana nanyi katika nyanja mbalimbali kwa kuwa tumeona matokeo chanya katika miradi ambayo benki hii imeiunga mkono hasa katika Sekta ya Nishati. “Alisema Makamba.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Seif Said na Mwakilishi wa



Waziri wa Nishati January Makamba, (katikati), Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati Kheri Mahimbali (wa tatu kulia) na Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia kwa upande wa Tanzania, Mara Warwick, (wa pili kushoto) wakizungumza wakati wa kikao cha kujadili maendeleo ya miradi ya Sekta ya Nishati, kilichofanyika mkoani Dar es Salaam, Machi 28, 2022.

# Waziri Makamba na Benki ya Dunia wajaadili maendeleo Sekta ya Nishati



Waziri wa Nishati, January Makamba, (katikati) akizungumza na ujumbe kutoka Benki ya Dunia, Viongozi waandamizi kutoka Wizara ya Nishati, Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakati wa kikao cha kujadili maendeleo ya miradi ya Sekta ya Nishati nchini, kilichofanyika mkoani Dar es Salaam, Machi 28, 2022.



Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati Kheri Mahimbali (wa pili kushoto) na Kamishna Msaidizi Maendeleo ya Umeme Wizara ya Nishati, Mhandisi Styden Rwebangila (kushoto) wakiwa katika kikao cha kujadili maendeleo ya miradi ya Sekta ya Nishati, kilichofanyika mkoani Dar es Salaam, Machi 28, 2022.

Mkurugenzi Mtendaji  
Shirika la Umeme  
Tanzania (TANESCO),

Anitha Ishengoma  
pamoja na Viongozi  
wengine waandamizi

kutoka wizarani, REA na  
TANESCO.  
Kikao hicho kilijadili

mradi wa Usambazaji wa  
umeme vijijinj, njia kuu  
za kusafirisha umeme  
pamoja masuala ya gesi.



Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Seif Said, (kushoto) na Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Jones Olotu, wakiwa katika kikao cha kujadili maendeleo ya miradi ya Sekta ya Nishati, kilichofanyika mkoani Dar es Salaam, Machi 28, 2022.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkazi wa WB nchini Tanzania, Warwick alimueleza Waziri wa Nishati kuwa wataendelea kushirikiana na serikali ya Tanzania kwa kuiunga mkono Sekta ya Nishati, ili kutanua wigo wa ukuaji ya sekta hiyo.

Aliongeza kuwa, watawajengea uwezo wataalam katika Sekta ya Nishati ili kuweza kuongeza tija na ufanisi katika sekta hiyo.

# Naibu Katibu Mkuu Nishati akagua miundombinu ya Gesi Songosongo



## **Na Zuena Msuya, Lindi**

**N**aibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali ametembelea na kukagua miundombinu ya Mradi wa kuzalisha na kuchakata Gesi asilia wa Songosongo uliopo Mkoani Lindi.

Mahimbali amesema kuwa lengo la ziara hiyo iliyofanyika Machi 31, 2022 ni kutaka kuona

shughuli za uzalishaji, uchakataji na usafirishaji wa Gesi asilia kutoka katika visima vya Gesi vilivyopo katika eneo la bahari nan chi kavu katika eneo hilo.

Katika ziara hiyo ametembelea mitambo ya kuchakata gesi asilia ya Songosongo, eneo ililofungwa mtambo mpya wa kuongeza mgandamizo wa Gesi asilia, pamoja na Kisima namba kumi (10) kinachofanyiwa ukarabati.

Aidha alitembelea kisima namba nne (4),(12), 11 pamoja na sehemu ambayo gesi inayozalishwa kutoka visimani inasafirishwa kuingia katika bomba la kusafirisha Gesi asilia kwenda Somangafungu hadi Kinyerezi, Dar es salaam kwa ajili ya kuzalisha Umeme na matumizi mengine.

Eneo lingine alilotembelea ni eneo la kupokelea gesi kutoka katika visima vya gesi inapochakatwa,

sehemu ya kuongeza mgandamizo wa gesi asilia (compression) pamoja na chumba maalum cha kuendesha mitambo ya gesi asilia (Control room).

Katika ziara hiyo ameambatana na Viongozi waandamizi kutoka Wizarani na Kampuni Tazuu ya kusimamia Gesi(GASCO) ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).





*Picha mbalimbali zikimuonyesha Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, akiwa katika ziara ya kukagua miundombinu ya mradi wa gesi asilia ya Songosongo mkoani Lindi.*

# Vijiji 25 Biharamulo kufikiwa na huduma ya umeme



Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato akizungumza na wananchi wa wilaya ya Biharamulo katika kijiji cha kalenge siku ya tarehe 02 machi 2022 " Serikali imeendelea kupeleka umeme katika maeneo yasiyokuwa na umeme, lengo likiwa ni kusukuma shughuli za maendeleo kwa Jamii ya watu waishio Vijijini".

Mwananchi wa Kijiji cha Mavota Bi. Esteria Mwesogwa kilichopo wilaya ya Biharamulo, wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Nishati, iliyofanyika tarehe 02 machi 2022, akiwasilisha ombi la kupatiwa umeme wa uhakika kutoka TANESCO katika kijiji cha Mavota ili kuondokana na changamoto ya upatikanaji wa umeme, kijiji hicho kinapata umeme kutoka kwa kampuni BINAFSI ya Powergen (umeme Jua).

## **Na Timotheo Mathayo, Biharamulo.**

**S**erikali imeendelea kupeleka umeme katika maeneo yasiyokuwa na umeme, lengo likiwa ni kusukuma shughuli za maendeleo kwa Jamii ya watu waishio vijijini.

Kauli hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato wakati alipofanya ziara ya kukagua miradi ya Umeme katika Vijiji vya Nyantakara, Mavota na Kalenge vilivyopo wilaya ya Biharamulo Mkoani Kagera.

Ziara hiyo imefanyika Machi 2, 2022 ambapo amewaambia wakazi wa vijiji hivyo kwamba watapewa umeme wa uhakika ili kuepuka kukosekana kwa huduma ya umeme usiokuwa na uhakika.

Akiwa katika kijiji cha Mavota amewaagiza TANESCO watumie miundombinu iliyokuwa inatumiwa na kampuni ya Powergen ili wakazi wa kijiji hicho waweze kupata umeme wa uhakika.

Mbunge wa jimbo la Biharamulo, Ezra Chiwelesa amesema wakazi wa vijiji vya Nyantakara, Kalenge na Mavoto wamekosa umeme wa uhakika kwa sababu kampuni ya powergen haitoi umeme wa uhakika.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Biharamulo, Leo Rushahu ameomba serikali ikamilishe utaratibu wa kupeleka umeme wa uhakika katika Vijijini vyote visivyokuwa na umeme, ikiwemo vinavyotumia umeme kutoka kampuni binafsi ya Powergen.

Mhandisi wa mradi wa REA kanda ya Ziwa, Ernest Makale amesema kuwa katika wilaya ya Biharamulo kuna vijiji 75 ambapo vijiji 50 vimepata umeme wa uhakika lakini vijiji 25 vipo kwenye mpango wa kuunganishiwa umeme kupitia REA.

Amesema changamoto ya bei na kukosekana kwa umeme wa uhakika itamalizika hivi karibuni katika vijiji vyote vya wilaya ya Biharamulo.

Wakazi wa kata ya Kalenge wameomba Serikali kupeleka umeme wa uhakika ili waondokane na adha ya kutegemea umeme unaozalishwa na kampuni binafsi ya Powergen inayotumia nishati ya Jua kuzalisha umeme.

Naibu waziri amewaambia wakazi wa kata ya Kalenge kwamba ujenzi wa kituo cha

# Vijiji 25 Biharamulo kufikiwa na huduma ya umeme



Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato (wa pili kutoka upande wa kushoto), akisikiliza kero kutoka kwa wananchi wa kijiji cha Nyankatara kilichopo katika wilaya ya Biharamulo siku ya tarehe 02 machi 2022 alipofanya ziara ya ukaguzi wa maendeleo ya miradi ya umeme ya Nishati Jadidifu.

kupoza umeme cha Nyakanazi kimekamili kwa zaidi ya asilimia 90.

Kabla ya mwezi wa sita mwaka huu vijiji vyote saba vilivyopo katika kata ya Kalenge vitakuwa vimepata umeme wa uhakika kupitia umeme wa gridi ya Taifa.

Byabato amesema kuwa gharama ya kuunganisha umeme katika kila kijiji ni sh. 27,000 na akitokea mtu yoyote akataka kuwaunganisha umeme

kwa zaidi ya bei hiyo hiyo taarifa zitolewe haraka.

Amesema kampuni ya Powergen itaendelea kutoa huduma ya umeme katika kata ya Kalenge mpaka pale umeme wa gridi utakapopelekwa katika kata hiyo.

Amewahakikishia kwamba TANESCO itapeleka nguzo za umeme kuanzia wiki ijayo na zitasambazwa katika vijiji vyote vya kata ya Kalenge.



Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati, Mhe. Stephen Byabato akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mavota kilichopo wilaya ya Biharamulo, wakati alipofanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya umeme, tarehe 02 machi 2022 na kuiangiza TANESCO kutumia miundombinu iliyokuwa ikitumiwa na kamupuni ya Powergen ili kuwasambazwa wananchi wa Mavota umeme wa uhakika kutoka TANESCO"

# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



**Fika Ofisi ya Mawasiliano,**  
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au  
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018  
**Nukushi** +255-26-2320148

 [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

 [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara.ya.Nishati)

 [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017)

 [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania)

 [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara.ya.Nishati)